# Shule na elimu

## Shule ya Kulea Watoto na Elimu ya Chekechea

Nchini Ufini watoto wengi walio chini ya umri wa kwenda shule husajiliwa kwenye chekechea zinazolea watoto kutwa kwa sababu mara nyingi wazazi hufanya kazi mbali na nyumbani. Kama mkazi wa manispaa, unaweza kutuma maombi ya nafasi ya watoto wako. Katika vituo vya kulea watoto wanajifunza lugha ya Kifini, nyimbo za kila siku na ujuzi muhimu wa maisha. Shughuli za kila siku za vituo hivi ni pamoja na michezo, kufanya mazoezi, muziki, sanaa na chakula cha pamoja. Watoto hucheza michezo ya nje na ya ndani bila kujali msimu. Ada ya vituo vya kulea watoto hutegemea pato la familia.

Mara nyingi watoto hucheza nje wanapokuwa kwenye vituo vya kulea watoto na wazazi wanafaa kuwavalisha nguo kulingana na hali ya hewa. Wanahitaji nguo zinazofaa ndani na nje ya nyumba.

Watoto wana haki ya elimu ya chekechea kwa kipindi cha mwaka mmoja kabla ya kuanza elimu ya msingi, kwa kawaida wanapotimu umri wa miaka sita. Manispaa yanaandaa mtaala wa elimu ya chekechea kwa watoto wanaostahiki. Katika elimu ya chekechea, watoto watapata maarifa na ujuzi ambao utawasaidia katika mchakato wao wa kusoma shuleni.

## Shule ya Kati

Masomo nchini Ufini hudumu kwa muda wa miaka 9 kwa elimu ya msingi. Watoto wote wanaoishi nchini Ufini wanawajibishwa kupata elimu ya msingi ambayo ni ya lazima. Wajibu huu huanza wanapokuwa na umri wa miaka saba na humalizika baada ya kumaliza silabasi ya lazima ambayo ni umri wa miaka 16. Wazazi wana wajibu wa kuhakikisha kwamba watoto wao wanaenda shuleni kila siku.

Shule ni pamoja na elimu ya shule ya msingi, sekondari ya awali. Shule ya msingi inaanza darasa la 1 hadi la 6 na sekondari ya awali huanzia darasa la 7 hadi 9.

Watoto husoma masomo mengi ya lazima shuleni kama vile Hesabu, Lugha ya Kifini, Kiingereza, historia, bayolojia, n.k. Wanafunzi wote nchini Ufini hushiriki katika elimu ya mazoezi ya mwili na masomo ya sanaa. Kuna kazi nyingi za sanaa na mikono shuleni na nyenzo za kuona hutumika sana katika kufundisha. Mwanafunzi huinua mkono wake anapoomba ruhusa ya kuzungumza darasani. Aidha lugha mbalimbali hufundishwa shuleni.

Wanafunzi hupewa shuleni nyenzo kama vitabu, penseli, vifutio n.k. bila malipo yoyote. Aidha wanafunzi hupewa chakula cha mchana bila malipo yoyote. Huduma hizi huwa zimelipiwa kutokana na mfuko wa kawaida, yaani kodi.

Ni lazima ugharimie vifaa vya shule kama vile mikoba, mifuko ya kalamu, na mavazi kwa ajili ya hali mbalimbali za hewa na madarasa. Wanafunzi nchini Ufini hawana sare ya shule, kwa hivyo wazazi wanawajibika katika kuhakikisha watoto wao wamevaa mavazi yanayofaa na nguo zinazofaa kwa hali ya hewa. Kwa masomo ya michezo na mazoezi, wanafunzi wanafaa kuwa na nguo na viatu vya michezo.

Mara nyingi somo huwa ni kipindi cha dakika 45. Ili kuwatia hamasa na kuhimiza umakini darasani huwa kuna dakika 15 za mapumziko baina ya vipindi. Wanafunzi huenda uwanjani wakati wa mapumziko kucheza na kujumuika katika matembezi.

Kwa sababu ya hali ya hewa wanafunzi huvua viatu vyao kwenye ushoroba wanapoingia kwenye jengo la shule. Hakuna mwanafunzi anayeruhusiwa kutoka bila nguo na viatu vya baridi.

Watoto wa wahamiaji ambao ndio kwanza wamewasili Ufini wanapewa mafunzo ya kujiandaa yanayowaandaa kabla ya kujiunga na shule. Wanafunzi husoma Lugha ya Kifini na masomo mengine na kuimarisha ujuzi wao wa kusoma na kuandika.

Nchini Ufini, mtoto wa mhamiaji huwekwa katika darasa linalofaa kwa umri, elimu na ujuzi alionao. Aidha, utaratibu wa kufundisha katika lugha nyingine unawezekana kwa wageni. Manispaa yanaweza kuwapa watoto wa wahamiaji elimu katika lugha zao ya kwanza.

Dini ni mojawapo wa somo katika shule ya kati na shule ya upili ya Ufini. Mafunzo yake hutolewa kulingana na wingi wa wafuasi wa dini. Wazazi wana haki ya kuomba elimu inayozingatia mafunzo ya dini yao.

## Shule ya Upili ya Juu

Mtu anaweza kutuma maombi ya elimu ya sekondari kwa kutumia cheti cha shule ya msingi kutoka kwenye shule ya kati. Elimu katika ngazi ya sekondari ya juu ni pana na ya kinadharia zaidi. Mtaala unajumuisha masomo ya jumla kama vile lugha, historia, saikolojia, hesabu, fizikia na kemia. Masomo yanaweza kukamilika kwa kipindi cha miaka 2-4 na huwa na mtihani wa kitaifa ambao huuliza maswali ili kutathmini maarifa kwa upana. Baada ya kuhitimu sekondari ya juu mwanafunzi hupata stashahada. Baada ya kufanikiwa katika mtihani wa kujiunga na chuo, mwanafunzi hupokea cheti cha

mtihani wa kujiunga na chuo. Elimu ya sekondari humwandaaa mwanafunzi kwa ajili ya elimu ya ngazi ya juu.

## Elimu ya Juu na Vyuo Vikuu

Mtu anaweza kupata elimu ya juu katika vyuo vikuu vya sayansi tumizi au katika vyuo vingine vikuu. Elimu katika vyuo vikuu vya sayansi tumizi vinasisitiza sana katika taaluma. Mtu anaweza kukamilisha elimu yake katika kipindi cha miaka 3 hadi 4 au 5. Kigezo cha kusajiliwa katika chuo kikuu ni kuwa na cheti cha elimu ya sekondari au chuo cha ufundi.

Vyuo vingi nchini Ufini vina mitaala ya sayansi. Shahada nyingi za vyuo vikuu ni Shahada ya kwanza ikifuata Shahada ya Uzamili. Vyuo vikuu vingi hufundisha katika shahada katika lugha ya Kiingereza.

## Elimu ya Maandalizi ya Ufundi kwa Vijana Wahamiaji

Baada ya kumaliza elimu ya msingi mtu anaweza kuamua kujiunga na elimu ya ufundi au shule ya upili ya juu. Ikiwa kijana mhamiaji anahitaji elimu zaidi katika Lugha ya Kifini au masomo mengine ya msingi, anaweza kujiunga na darasa la 10 katika elimu ya msingi au mwaka mmoja katika mafunzo ya ufundi.

Katika elimu ya maandalizi ya ufundi mwanafunzi huimarisha ujuzi wake wa lugha ya Kifini, hupata ujuzi wa maisha na taaluma mbalimbali, na hujiandaa kwa ajili ya elimu ya ufundi. Wakati wa mafunzo ya maandalizi mwanafunzi atapata fursa wa kutambua uwezo na matamanio yake katika taaluma.

## Elimu na Mafunzo ya Ufundi

Kuna vyuo vingi vya ufundi nchini Ufini vinavyotoa mafunzo katika kozi mbalimbali za ufundi zinazompa mwanafunzi ujuzi wa kuhitimu katika taaluma ya ufundi. Katika elimu ya ufundi kijana anaweza kuhitimu na kupata ujuzi wa ufundi, elimu hii huchukua takribani miaka 2 hadi 3. Elimu ya ufundi ni muhimu sana. Wanafunzi wanakuwa na madarasa mengi ya ujuzi halisi katika sehemu za kazi mbalimbali. Mtu anaweza kutuma barua ya kujiunga na chuo cha ufundi kwa kutumia cheti cha shule ya msingi au cheti sawa na elimu ya shule ya msingi. Kwa sababu lugha ya kufundishia katika vyuo vya ufundi ni Kifini, ni muhimu kwa wenye nia ya kujiunga na vyuo vya ufundi kujifunza lugha ya Kifini mapema iwezekanavyo.

## Mafunzo ya Kutangamana na Jamii kwa Wahamiaji

Baada ya kuwasili nchini Ufini, wahamiaji husajiliwa katika mradi wa kuwapa mafunzo ya kutangamana ambayo ni pamoja na lugha ya Kifini, elimu ya jamii, ujuzi wa maisha ya kila siku, elimu ya utamaduni kadhalika ushauri kuhusu elimu na ushauri nasaha na elimu ya juu na ajira. Aidha, mradi huu una masomo yanayofanyika kazini. Kwa kawaida mafunzo ya kutangamana hudumu kwa kipindi cha mwaka mmoja. Wakati wa mafunzo haya ni muhimu kuwa na mkakati wa elimu yako ambayo itakusaidia kupata ajira nchini Ufini.

## Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa Watu Wazima

Sawa na wahamiaji vijana, wahamiaji watu wazima wanaweza pia kutuma maombi ya elimu na mafunzo ya ufundi ili kupata uhitimu wa kitaalamu unaohitajika katika masoko ya kazi nchini Ufini. Anayetuma maombi anastahiki iwapo ana cheti kutoka kwenye shule ya msingi au cheti sawa cha elimu, aidha awe na ujuzi wa kutosha katika lugha ya Kifini. Unahimizwa kuhitimu shahada yako ya ufundi nchini Ufini kwa sababu inaimarisha nafasi ya mhamiaji katika soko la ajira. Ni muhimu kupata taarifa kuhusu fursa za elimu ya ufundi katika mkoa unaoishi nchini Ufini.

## Mafunzo ya Soko la Ajira kwa Watu Wazima

Wahamiaji ambao hawana kazi na ambao wamekamilisha mafunzo ya kutangamana na kuwa na ujuzi wa lugha ya Kifini inayohitajika katika elimu ya ufundi, wanastahiki kwa mafunzo ya soko la ajira. Mafunzo ya soko la ajira ni ya nyanjani na yanajumuisha masomo kadhaa na mara nyingi humwezesha mtu kuhitimu katika taaluma ya ufundi.

## Kuthibitishwa kwa Elimu na Shahada za Nje ya Nchi

Mfumo wa elimu wa Ufini unalenga kwamba shahada ya mtu, elimu au uzoefu alionao katika taaluma kutoka nchi nyingine ni msingi wa kuweka mikakati ya elimu yake ya juu nchini Ufini. Iwapo mhamiaji amehitimu shahada nje ya nchi, anaweza kutuma maombi ya kuthibitishwa nchini Ufini katika Bodi ya Elimu ya Ufini (FNBE).

Bodi ya FNBE huidhinisha ustahiki wa shahada katika muktadha wa masoko ya ajira ya Ufini na huamua elimu ya juu anayohitaji mhamiaji. Ili kuwawezesha wahamiaji wenye uzoefu kuendeleza

taaluma zao katika maisha yao ya kufanya kazi nchini Ufini kuna mafunzo ya kozi za kitaaluma yanayotolewa nchini. Kozi hizi ni pamoja na zinazohusu mafunzo ya wauguzi.

Wahamiaji wote wanapohamia Ufiniwanapaswa kubeba vyeti vyao vilivyoidhinishwa vya elimu ya msingi, mafunzo ya vyuo anuwai, shahada na stakabadhi za uzoefu wa kazi. Vitakuwa vizuri zaidi kama tayari nakala hizi zimetafsiriwa katika lugha ya Kiingereza kutoka nchi zinakotoka.

## Maktaba

Manispaa meingi nchini Ufini yana maktaba ya umma, ambayo yanaweza kutumiwa na wananchi wote. Mtu anaweza kuazima vitabu kama vile majarida mbalimbali katika lugha. Mteja anaweza kutumia intaneti na kusoma maktabani. Ili uazime vitabu katika maktaba unapaswa kujisajili ili upate kadi ya maktaba.